BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MIUNDOMBINU, ARDHI NA TEHAMA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezimungu Mtukufu mwingi wa rehma kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Baraza hili tukufu kujadili na kupitisha Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka Fedha 2026/2027. Tunaomba Rehema za Mwenyezi Mungu ziendelee kutushukia ili tuweze kutimiza majukumu yetu ya msingi ya kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati nichukuwe fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** Raisi wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi**, Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwao tena na wananchi katika uchaguzi Mkuu uliopita wa Octoba 2025 ili kuendelea kuongoza nchi yetu kwa kipindi cha pili katika uongozi wao, Tunawaombea kwa Mola mtukufu awazidishie afya njema na maisha marefu ili waweze kuendeleza Kuliongoza Taifa kwa salama na Amani na kutuletea

maendeleo zaidi nchini mwetu.

**Aidha,** tunatoa pongezi za dhati kwa **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa kuchaguliwa na wananchi kwa nafasi ya Uwakilishi jimbo la Kiwani na pia kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar kuwa Makamo wa Pili wa Raisi na kuwa Mkuu wa shughuli za Serikali katika chombo hiki muhimu cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe Fursa hii Kukupongeza wewe binafsi Spika wa Baraza la Wawakilishi, **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** kwa kuchaguliwa tena na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kwa nafasi ya Spika. Namuomba Allah (sw) akuzidishie hekma na busara katika kutuongoza kwako na pia nikushukuru kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha hotuba hii ya maoni na ushauri wa Kamati ya kudumu ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Aidha,** Nichukuwe nafasi hii tena kuwapongeza wasaidizi wako, Naibu Spika Mheshimiwa **Mwanaasha Khamis Juma** pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa pamoja kwa kuchaguliwa kwa nafasi zao hizo ili kutuongoza katika Baraza hili tukufu na kwa kipindi cha muda mfupi tu tokea kuteuliwa kwenu tunaona mnaliendesha kwa umahiri Mkubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Sina budi pia kumshukuru Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Zanzibar, **Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohamed,** pamoja na Naibu Waziri **Mheshimiwa Badria Attai Masoud**, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia Kamati yetu wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara yao.

**Mheshimwa Spika,** Kwa niaba ya wajumbe wengu wa kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa kwao kwa nafasi tofauti kuwa wajumbe katika Baraza hili Tukufu kwa kipindi hiki cha miaka mitano, Tunamuomba Allah atujaalie mashirikiano na wepesi katika kutekeleza majukumu yetu tunayopaswa kuyatekeleza kikatiba.

**Mheshimwa Spika,** pia niwashukuru Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza **Ndg. Raya Issa Msellem** kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia Kamati yetu kwa lengo la kufanikisha shughuli za Baraza za kuisimamia Serikali katika utendaji kazi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Shukran za pekee nazitoa kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama ambao kwa pamoja tumeweza kujadili kwa kina makadirio ya Bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi na kuhoji mipango mbali mbali ya Wizara kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinishiwa zinatumiwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Heshima kubwa naomba niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mihayo Juma N'hunga | Mwenyekiti. |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Makamu Mwenyekiti. |
| 3. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe. |
| 4. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe, |
| 5. | Mhe. Khamis Mohammed Amran Hijaz | Mjumbe, |
| 6. | Mhe. Abdullah Kambotwe Abdullah | Mjumbe, |
| 7. | Mhe. Said Ali Mbarouk | Mjumbe, |
| 8. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu, |
| 9. | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu, |
| 10. | Ndg. Adam Maulid Simai | Afisa Bajeti. |

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika kanuni ya 101 fasili ya kwanza ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024, Kamati ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kama ifuatavyo;

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yenye fungu **061** ina jumla ya Program kuu tatu na program ndogo saba pamoja na Taasisi

Kumi zinazojitegemea ambazo kwa pamoja zimeweza kuunda Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo awali ilijulikana kama Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, ilikadiriwa kukusanya jumla ya mapato ya **Shilingi Bilioni tano, Milioni Mia Mbili na Nne, Laki Tisa na Ishirini Elfu (5,204,920,000),** hadi kufikia Machi 2026, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Sita, Laki Tisa Themanini na Nane Elfu, Mia Moja na Sabiini na Moja na Senti Saba (2,006,988,171.7) Bilioni** sawa na **asilimia 38** ya makadirio ya mwaka.
Kadhalika, Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tano Kumi na Moja, Milioni Mia Tano Sabiini na Nane, Laki Moja Sabiini na Nane Elfu, Mia Tano na Kumi na Tano (1,511,578,178,515) ambapo** hadi kufikia Machi 2026, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imetumia jumla ya **TZS Bilioni Mia Nane Sabiini na Sita, Milioni Mia Tatu Themanini na Tano, Laki Nne Thelathini na Sita, Mia Moja na Ishirini na Tatu na Senti Moja (876,385,436,123.1)** sawa na **asilimia 58** ya makadirio ya mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekadiriwa kutumia ***Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Kumi na Tano, Milioni Mia Tatu na Kumi na Laki Tatu (1,815,310,300,000)*** na imekadiriwa kukusanya shilingi ***Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Sabiini na Tano (5,275,000,000),*** Kamati inaiomba Serikali kuipatia fedha za matumizi kama zilivokadiriwa kwa Wizara hii muhimu ili kuweza kutekeleza Majukumu waliojipangia kwa ufanisi ikiwemo miradi ya maendeleo

ukizingatia kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara hii ndio kiungo muhimu katika kutekeleza adhma ya serikali katika utarajishaji wa mashindano ya kombe la mataifa Afrika (AFCON) ambapo Zanzibar ni mmoja wa wenyeji wa michuano hiyo.

PROGRAMU KUU YA UJENZI NA MIUNDOMBINU YA BARABARA (P01)

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuanzia na program kuu ya ***Ujenzi na Miundombinu ya Barabara (P01)*** yenye program ndogo mbili ambayo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepangiwa kutumia ***Trilioni Moja, Bilioni Mia Tatu na Ishirini,Milioni Mia Moja na Tisini na Moja, Laki Tano na Arubaini Elfu (1,320,191,540,000),*** Kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya nane kwa kufanikisha kwa kiwango cha juu ujenzi wa barabara kwa Unguja na Pemba zenye ubora na hadhi katika maeneo ya Mijini na Vijijini, hatua hii imepelekea kupanua maendeleo kwa nchi yetu na kuongeza nafasi kwa wawekezaji mbali mbali wa ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika program ndogo ya Kwanza ya ***Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara*** **(S0104)** iliyokadiriwa kutumia ***Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tatu Kumi na Nne, Milioni Mia Nne Hamsini na Nne, Laki Tisa na Themanini Elfu (1,314,454,980,000)*** kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuboresha miundombinu ya barabara, katika utekelezaji wa program hii kamati inaendelea kusisitiza suala zima la usimamizi na utunzaji wa miundombinu ya barabaraza zetu ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa na fedha nyingi za Serikali na wafadhili kwa kuzitunza, na kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya barabara pamoja na miundombinu yake ili kuepusha uharibifu

usiokua wa lazima.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala wa Barabara Zanzibar alikadiriwa kutumia jumla ya TZS. **Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Sita Na Arubaini na Nne, Laki Nne na Ishirini na Nnne Elfu (18,644,424,000)** ambapo hadi kufikia Machi 2026 kamati imearifiwa kwamba jumla ya **Bilioni Saba, Milioni Mia Tano na Tano, Laki Nne Kumi na Nne Elfu, Mia Tisa Sabiini na Saba (7,505,414,977)** zimepatikana, Hivyo kamati inashauri Serikali kwa mwaka wa fedha ujao kuwapatia Wakala wa Barabara fedha wanazokadiriwa ili waweze kutekeleza majukumu yao yakiwemo ukarabati wa Barabara kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara kwa barabara zetu za Mijini na Vijini kuwekwa alama za barabarani na kingo za barabara, kuziba mashimo, kuwekwa taa za kuongozea vyombo (traffic light) pamoja na kuwekwa taa za barabarani ambazo zitasaidia katika kupunguza ajali za barabarani pamoja na vitendo vya kihalifu vinavyofanyika hasa nyakati za usiku kwa kukosekana kwa taa za barabarani katika maeneo mengi mijini na vijijini. Lakini pia Kamati, inaishauri wizara kuwachukulia hatua kali wale wote watakaoharibu miundombinu ya barabara kwa mujibu wa sheria kwani hawana lengo jema kwa nchi yetu katika suala zima la maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Mbali ya hatua hiyo kubwa iliyofikiwa na Serikali katika ujenzi wa barabara, Kamati inashauri Wizara kuangalia uwezekano wa kuwafikia wananchi wanaoishi katika maeneo ya visiwa mfano kisiwa cha

Tumbatu, Njau, Kokota na Makoongwe kwa kuwajengea barabara na njia za watembea kwa miguu ili waweze kuishi katika mazingira bora na rafiki na kuweza kuzifikia huduma za kijamii kwa wepesi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika program ndogo ya ***Usimamizi wa Ujenzi na Majengo (S0105) ambayo imekadiriwa kutumia shilingi Bilioni 5,736,560,000*** kwa mwaka 2026/2027, kupitia program ndogo hii ambayo inasimamiwa na Wakala wa Majengo kamati inashauri Wizara kuwatumia kikamilifu wataalamu hao katika miradi ya Serikali kama wataalamu watasaidia katika kuondosha changamoto nyingi zisizo na lazima katika miradi ya Serikali kwa kupatikana miradi bora na yenye tija kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wakala wa Majengo wanafanya kazi kwa ufanisi mkubwa, kamati inashauri Serikali kuwapatia Wakala hao asilimia hamsini (50%) ya marejesho (retantion) ya Serikali ili kuzidisha hamasa kwenye utekelezaji wa kazi zao na kufikia malengo waliyopangiwa na pia itazidisha uchangiaji wa gawio kwa Serikali.

## PROGRAM KUU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA UCHUKUZI (P02)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa program Kuu ya ***Miundombinu na Huduma za Uchukuzi (P02),*** Kupitia programu hii kuu ambayo ndani yake ina program ndogo mbili (2), *Programu ya Usimamizi wa Miundombinu ya Uchukuzi* ***(S0201)*** *na Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama* ***(S0202)*** ambayo kwa mwaka wa fedha imepangiwa Shilingi **Bilioni Mia Nne Themanini na Nane, Milioni Mia Tatu Themanini na Saba, Laki Tatu na Sabiini Elfu (488,387,370,000)** ili kuweza

kutekeleza kazi zake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika program ndogo ya ***Usimamizi wa Miundombinu ya Uchukuzi (S0201),*** Kamati inaridhishwa na jitihada za Serikali kwa kupiga hatua kwenye miundombinu ya usafiri wa Anga na Baharini kwa Unguja na Pemba kwa ujenzi wa jengo la abiria Terminal II lilitengewa shilingi **Bilioni Thelathini (30,000,000,000)** pamoja na kujenga jengo jipya la kuongozea ndege (control tower) katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa AAKIA kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Lakini pia ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Pemba ambao umepangiwa kutumia shilingi **Bilioni Mia Moja Arubaini na Nne na Milioni Mia Tano (144,500,000,000**) miradi hii itakapokamilika na kuanza kazi italeta faida kubwa kwa Serikali lakini pia itakua faraja kwa watumiaji wa ndani na nje ya Zanzibar na kupiga hatua katika kukuza uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya ***Usimamizi wa utoaji wa huduma za Usafirishaji na Usalama****. (0202),* Programu hii inayosimamiwa na idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Kamati inashauri Wizara kuiangalia kwa jicho la karibu Karakana Kuu ya Magari kwa kuwaingizia fedha kikamilifu kwani kwa mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia Machi 2026 Wakala wameingiziwa **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Kumi na Tano, Laki Tano na Saba na Shilingi Kumi na Mbili nukta Tano (1,415,507,012.5)** sawa na asilimia 49.26 ya makadirio ya mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Ili Karakana Kuu iweze kufanya kazi kwa ufanisi inahitaji fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa pamoja na

uwendeshaji. Hivyo upungufu wowote wakifedha utakaojitokeza unapelekea Wakala kushindwa kununua vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Aidha Kamati inashauri  Wizara kuwapatia wataalamu wa ufundi wa magari na kuwajengea uwezo waliopo ili kufanikisha kazi zao kwa ufanisi.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (P03)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa ***Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya ujenzi na Uchukuzi*** (P03) yenye Programu ndogo tatu, Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imekadiriwa kutumia **Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Arubaini na Sita na Laki Nne (6,746,400,000)**

**Mheshimiwa Spika**, *Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji (S0301)***.** Kamati kupitia program hii inashauri wizara kutoa kipaumbele kwa watendaji kuwapatia mafunzo hasa kwa wale wa kada maalum za kitaalamu ili waweze kwenda sambamba na mahitaji ya taaluma zao na kuleta ufanisi kwa wizara na kuondokana na tabia ya kuchukua wataalamu kutoka nje ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa program ndogo ya ***Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara*** (S0302) Kamati inashauri Wizara kupitia program hii kuendelea kufanya tafiti za miradi iliyopo chini ya Wizara yake ambazo zitaweza kuboresha viwango vya miradi itayotekelezwa na wizara na kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi za Wizara. Kamati inaomba

Serikali kuwapatia fedha zilizokadiriwa katika program hii shilingi **Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Thelathini na Tisa, Laki Nane na Arubaini (1,539,840,000)** kwa mwaka wa fedha ujao ili waweze kufanikisha malengo yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya ***Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba (S0303).*** Kamati kupitia program hii inashauri Afisi ya Afisa Mdhamin Pemba kuratibu, kusimamia na kufatilia masuala yote ya Wizara hii kwa ufanisi ili kufikiwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati inaomba kuwapatia shilingi Bilioni 1,349,960,000 ili waweze kufanikisha malengo waliojipangia kwa ufanisi kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi zinazojitegemea ikiwemo Shirika la Meli, Shirika la Bandari, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Viwanja vya ndege, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani,Bodi ya Usajili wa Wawakandarasi na Bodi ya Usaji, Uhandisi na Wakadiriaji Majengo ni nyenzo muhimu katika kufanikisha malengo ya Wizara waliojipangia lakini kutokana na utaratibu uliopo sasa na kwa mujibu wa Takwa la Sheria Namba 6 ya Mwaka 2021 ya Msajili wa Hazina kifungu cha **26 (1) b,** Bajeti zake zinapitishwa na **bodi zao** na kamati haipati fursa ya kuzipitia lakini pia hata katika randama ya Wizara hazionekani, Kamati inashauri Serikali kuliangalia kwa kina suala hili kwani linaleta ukakasi pamoja na kuangaliwa kwa kuwekwa utaratibu maalum kwa Kamati kuzipitia bajeti za Taasisi hizo mara tu zinapoandaliwa ili kupata fursa ya kushiriki na kutoa ushauri kwa bajeti hizo.

## HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba yangu kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii kwani imebeba sekta muhimu sana za nchi yetu ambazo ndio mategemeo makubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………………………
Mheshimiwa Mihayo Juma N'hunga,
Mwenyekiti,
Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama,
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**